OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# WIKI HII KWENYE MAGAZETI NA MITANDAO

19/08/204 ► 23/09/2024

OAG

MAUA

KATIBU wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, akimkaribisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, alipomtembelea ofisini kwake bungeni jijini Dodoma, jana. (Picha na Ofisi Bunge).





Katibu Mkuu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi akimkaribisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari ofisini kwake kwa mazungumzo mjini Dodoma jana. (Picha na Bunge).

Jumanne Agosti 20, 2024 Nipashe 5

AIFA



Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, akizungumza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari alipomtembelea ofisini kwake Bungeni jijini Dodoma jana kwa lengo la kujitambulisha kwake baada ya kuapishwa na Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



oagtanzania www.oag.go.tz

DODOMA

Jumatano Agosti 21, 2024 Nipashe 15



# AG asisitiza kufanya kazi kwa weledi

Na Paul Mabeja, DODOMA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, amewataka watumishi wa ofisi hiyo kufanya kazi kwa weledi ili kuongeza ubora na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku ya kuwatumikia wananchi.

Alitoa wito huo juzi jijini hapa, wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya ofisi na aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jaji, Dk. Eliezer Feleshi.

Alisema watumishi wa ofisi yake wanapaswa kufanya kazi kwa weledi ili kuongeza ubora na ufanisi katika kuwahudumia wananchi wenye changamoto mbalimbali za kisheria.

"Niwaombe watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kufanya kazi kwa kuzingatia weledi ili kuongeza ubora na ufanisi wakati wa kutekeleza majukumu yenu ya kuwahudumia Watanzania," alisema Johari.

Aidha, aliitaka menejimenti na watumishi wa ofisi yake kufanya kazi kwa bidii, huku wakiifuata na kuiishi kauli mbiu ya ofisi hiyo ya weledi na ubora.

Katika makabidhiano hayo, Johari aliambatana na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Johari alimshukuru aliyekuwa mtangulizi wake, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Balozi Prof. Kennedy Gastorn, menejimenti na watumishi wa ofisi hiyo kwa mapokezo mazuri.

"Nawashukuru sana kwa mapokezi mazuri mliyonipatia kwa kifupi niwasisitizie kuwajibika kwenye majukumu yetu ili tufikie malengo yetu kwa kufuata misingi ya weledi na ubora," alisema.

Kadhalika, aliahidi ushirikiano kwa menejimenti na watumishi wa ofisi hiyo katika kufanikisha utelekezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno, akizungumza wakati wa hafla hiyo alisisitiza kufanya kazi kwa bidii ili kuyafikia malengo ya ofisi hiyo.

"Ofisi yetu hii ina majukumu makubwa na mteja wake namba moja ni serikali kwahiyo ili kufanikisha na kuifikia kauli mbiu yetu ya weledi na ubora kutatokana na ushirikiano baina yetu ninyi na sisi," alisema.

Kwa upande wake Jaji Dk. Eliezer Feleshi aliwapongeza kwa kupata uteuzi huo na kuwaahidi ushirikiano kwenye masuala mbalimbali kila itakapohitajika.

Kadhalika, aliitaka Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuwapa ushirikiano viongozi hao.

Alisema: "Niwapongeze sana kwa kupata uteuzi huu na nina imani mtaifanya ofisi hii kuwa juu zaidi kwenye kuisaidia serikali, hapa tuna timu nzuri ya menejimenti niwaombe wajumbe wa menejimenti kuwapa ushirikiano viongozi hawa ili watekeleze majukumu yao vizuri na kwa ufanisi".

# Mwanasheria Mkuu asisitiza kazi kwa weledi

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari ameitaka menejimenti na watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya kazi kwa bidii wakichagizwa na falsafa ya ofisi hiyo ya weledi na ubora.

Johari alitoa rai hiyo wakati wa ukaribisho na kusisitiza wajumbe wa menejimenti kuendelea kufanya kazi kwa bidii wakichagizwa na falsafa ya weledi na ubora.

"Nawashukuru sana kwa mapokezi mazuri mlionipatia, kwa kifupi niwasisitizie kuwajibika kwenye majukumu yetu ili tufikie malengo yetu kwa kufuata misingi ya weledi na ubora," alisema.

Aliahidi pia kuipa ushirikiano menejimenti na watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa upande wake, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno alisema ufanyaji kazi kwa bidii utachangia ofisi hiyo kufikia malengo yake.

"Ofisi yetu hii ina majukumu makubwa na mteja wake namba moja ni serikali kwa hiyo ili kufanikisha na kuifikia kaulimbiu yetu ya weledi na ubora unatakiwa ushirikiano baina yetu na ninyi," alisema.

Awali aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye sasa ni Jaji wa Mahakama ya Rufani, Dk Eliezer Feleshi aliwapongeza viongozi hao kwa kupata uteuzi huo na kuwaahidi ushirikiano kwenye masuala mbalimbali kila itakapohitajika.

Aliitaka pia menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuwapa ushirikiano viongozi hao wapya walioingia katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Niwapongeze sana kwa kupata uteuzi huu na ninaimani mtaifanya ofisi hii kuwa juu zaidi kwenye kuisaidia serikali, hapa tunatimu nzuri ya menejimenti, niwaombe wajumbe wa menejimenti kuwapa ushirikiano viongozi hawa ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri na kwa ufanisi," alisema.

Katika hatua nyingine, aliyekuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye sasa ni Mshauri wa Rais, Sheria na Mikataba, Balozi Profesa Kennedy Gastorn aliiomba menejimenti ya ofisi hiyo kuendelea kutoa ushirikiano kwa viongozi wapya kama ambavyo walikuwa wakifanya chini ya uongozi uliopita.

"Kama ambavyo mlinipokea mimi na kunipa ushirikiano kwenye masuala mbalimbali basi nawaomba ushirikiano uleule muendeleze kwa kuwapatia viongozi hawa wapya ili watekeleze majukumu yao," alisema.

Naye Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njole aliahidi kuwa menejimenti itatoa ushirikiano.

Baada ya kikao hicho Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali walikabidhiwa nyaraka na kutembelea ofisi.

**OAG Tanzania**
3d ·

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI ASISITIZA UWAJIBIKAJI, WELEDI NA UBORA··· See more




See insights and ads

Boost post

3

1 share

FULLSHANGWE blog

CONTACT:
phone: +255 713 410 6
+255 755 333 3
P.O BOX 78392, Dar es Sala
Email. johnbukuku@gmail.c

Home Biashara Burudani Magazeti Mchanganyiko Michezo Siasa Teknolojia TV Makala

MCHANGANYIKO

# WATUMISHI OFISI YA MWANASHERIA MKUU WATAKIWA KUFANYA KAZI KWA WELEDI

Alex Sonna · 4 days ago
Last updated: 2024/08/19 at 4:14 PM

Share





oagtanzania www.oag.go.tz

oagtanzania

MATUKIO KATIKA PICHA WAKATI WA HAFLA YA MAPOKEZI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI NA NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI, MTUMBA JIJINI DODOMA TAREHE 19 AGOSTI, 2024













**OAG Tanzania**

2d ·

KAMATI ZA KISHERIA ZA MIKOA NA WILAYA KUENDESHA KLINIKI YA KISHERIA··· See more



**OAG Tanzania**

11h ·

HABARI PICHA

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bw. Hamza Johari amehudhuria uzinduzi wa Jarida la Marekebisho ya Sheria (Law Reforms Journal) lililoandaliwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, uzinduzi huo umefanyika tarehe 21 Agosti 2024 Jijini Dodoma.



OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

# TUPO KARIBU YAKO!

## Tufuatilie kupitia

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora